

***'Unspoken Words'* ni Kitabu cha Kwanza Alichochapisha  
Mwanafunzi wa Shule ya Clarkston HS; Sasa Kinapatikana katika  
Amazon**

Wakati mwanafunzi wa mwaka wa mwisho katika Shule ya Clarkston High, Kira Farris alipokuwa akikabiliana na hali ngumu iliyohusisha mvulana miaka michache iliyopita, aliamua kuelekeza hasira zake na hisia zingine katika kuandika mashairi.

[\*The Unspoken Words\*](#) ni kitabu cha mashairi cha kurasa 101 chenye sura nane zinazoangazia mada za kuvunjika moyo, kazi na kujigundua. Kilichapishwa tarehe 26 Desemba 2023.

“Mashairi haya yanasimulia kisa cha maisha yangu nikiwa mdogo na jinsi nilivyokuwa katika hali ngumu na kuruhusu mvulana mpumbavu kunifanya niwe na tabia zisizofaa ambazo zilinitenganisha na watu wa karibu,” alisema Kira. “Jambo zuri ni kwamba niliweza kugundua hili na kujiondoa. Kwa msaada wa mamangu, mshauri na familia na marafiki zangu, niliweza kupona kutokana na hayo yote.”

Shule ya Clarkston High iliandaa hafla ya kutia saina kitabu na kukutana na kusalimiana katika kituo cha habari cha shule mnamo tarehe 29 Februari ili kusherehekea mafanikio ya Kira. Hata aliandaa kikao cha Maswali na Majibu kuhusu kitabu chake na kushiriki motisha na safari yake kama mwandishi mpya. Pia alitia saina nakala za kitabu chake kwa wanafunzi, kitivo na wafanyakazi. Kira alionyesha msisimko wake na pia kuchanganyikiwa kuhusiana na kuwa mwandishi aliyechapisha kazi yake.

“Sikuwa na nia yoyote ya kuyachapisha mashairi mwanzoni. Niliandika kitabu hiki ili kuwa na kumbukumbu ya mawazo yangu, na nilitaka kipindi hicho cha maisha yangu kisahaulike,” alisema Kira. “Nilipochapisha kitabu, nilifikiri labda hadithi yangu inaweza kumsaidia mtu mwingine.”

Kira amekuwa akiandika kwa miaka mitatu, na kuandika kitabu cha [\*The Unspoken Words\*](#) ilimchukua takriban mwaka mmoja. Alichapisha mwenyewe kitabu chake kupitia Amazon KDP, ambayo huchapisha vitabu bila malipo. Kufikia sasa, ameua vitabu 32 na vinaendelea kununuliwa.

“Inanifanya nihisi vizuri kwamba watu wanasoma kitabu changu kwa sababu inanidhihirishia kuwa hadithi yangu imesikika,” alisema. “Ninaishukuru sana shule yangu, hasa Bi. Harden, kwa sababu sikukusudia kuiambia shule kuhusu kitabu changu. Bi Harden alipojua, alisema ni lazima tutie saina kitabu, na kila mtu akahusika.”

Tracie Harden, Mtaalamu wa Habari katika Maktaba ya Clarkston High School na pia mwandishi aliyechapisha kazi yake, alionyesha fahari yake kwa mafanikio makubwa ya Kira na alitaka kumsherehekea.

“Ingawa yeye ni mnyenyekevu, hili ni jambo kubwa,” alisema Bi. Harden. “Amechapisha kazi yake, na alikuwa jasiri na mkakamavu vya kutosha kuandika hadithi yake kwenye karatasi na kuishiriki na kila mtu.”

Kira anatarajia kuandika vitabu zaidi katika siku zijazo. Hata hivyo, kwa sasa, amejitolea kwa masomo yake. Atahudhuria Chuo Kikuu cha Savannah State kusomea ya sayansi ya uchunguzi, akilenga kuwa mpiga picha wa uchunguzi. Kira anasema kitabu chake kinalenga kutoa funzo muhimu.

“Natumai kuwa hakuna mtu atapuuza thamani yake,” Kira alisema. “Hiyo ni kwa sababu thamani ya mtu haipaswi kupimwa na mtu mwingine yeyote isipokuwa yeye mwenyewe.”

Ili kutazama picha kutoka kwa tukio la kutia saini kitabu, bofya [hapa](#).

XXX